SUALA LA MJONGEO KATIKA MASHAIRI YA KASWIDA ZA KISWAHILI: HALI NA MIFANO YAKE

Tatu Y. Khamis
Mhadhiri Msaidizi
Chuo Kikuu cha Dodoma
khamist910@gmail.com

IKISIRI

Suala la mjongeo katika fani za fasihi ya Kiswahili, sio geni sana kwa wanataaluma wa Kiswahili ingawa halijafanyiwa kazi vya kutosha. Hata hivyo, suala hili (la mjongeo) huangaliwa sana katika fani za nathari kama vile hadithi fupi na riwawa na fani za majibizano kama vile tamthiliya (Msokile, 1973; Mulokozi, 2017). Suala la mjongeo katika ushairi wa Kiswahili hususan kaswida, halijatazamwa kwa jicho la kubainishwa hali na mifano yake. Hivyo, makala hii inajikita kuelezea suala hili kwa jichola kipee. Hali zitakazochunguzwa ni hali ya kasi (haraka haraka) na hali ya upole (polepole). Aidha, vipengele vitakavyoshuhulikiwa kwa kuonesha mifano inayoibua hali hizo ni kama vile maradhi, maombi, vifo, mauaji na majanga kwa upande wa mjongeo wa polepole na kipenge cha pongezi, burudani, hamasa kwa hali ya mjongeo wa haraka haraka. Chanzo cha maarifa haya ni utafiti mdogo wa kimaktaba ambao umehusisha data za awali zilizopatikana kwa kusikiliza kaswida za Kiswahili na data za upili zilizopatikana kwa kusoma tahakiki, makala na tasnifu mbalimbali zilizochambua masuala ya mjongeo katika fani za fasihi. Uwasilishwaji wa data hizo, zitakuwa katika mkabala wa kitaamuli; hii ni kutokana na kuwa data hizi hazitajumuisha maarifa ya ukweli usiogawanyika. Hii ni kutokana na ukweli kwamba, mkabala wa kitaamuli unajihusisha na kweli nyingi ambapo masuala ya hali ya mjongeo inategemea mpokeaji wa kazi husika. Hivyo, huwezi kuijumuisha katika kweli isiyotawanyika ndio maana inaaminika kuwa kweli ya jambo hutegemea muktadha wa jambo hilo linapotokea.